**22E-Maddutw-Twabiy'iy - Maddul-'Iwadhw**

**iii- مَدُّ الْعِوَض Maddul-'Iwadhw**

Ni madd inayotokea wakati wa kusimama msomaji katika neno lenye fat-hataan (tanwiyn fat-hah). Hukmu yake ni huvutwa kwa harakah mbili.

Mfano:

﴿ ٱلَّذِى جَعَلَ لَكُمُ ٱلْأَرْضَ فِرَٰشًا وَٱلسَّمَآءَ بِنَآءً وَأَنزَلَ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً ..... ﴾[1]

Wakati wa kusimama kwenye neno فِرَٰشًا ; بِنَآء na مَآء hubadilishwa tan-wiyn ya fat-hataan na kuwa alif. Ama lnapounganishwa neno hutamkwa kutegemea na hukmu inayofuatia.

| Linapounganishwa hutamkwa kwa tanwiyn | Linaposimamiwa hubadilika tanwiyn ya fat-hataan na kuwa alif | Neno |
|---|---|---|
| sa'iyran | سَعِيرَا<br>**sa'iyraa** | سَعِيرًا |
| Rahiyman | رَحِيمَا<br>**Rahiymaa** | رَّحِيمًا |
| Hudan | هُدَا<br>**Hudaa** | هُدًى |
| musamman | مُسَمَّا<br>**musammaa** | مُّسَمًّى |
| nisaaaaan | نَسَآءَ<br>**nisaaaaa** | نِسَآءً |
| maaaaaa | مَآءَ<br>**maaaaaa** | مَآءً |
| afwaajan | أَفْوَاجَا<br>**afwaajaa** | أَفْوَاجًا |

[1]Al-Baqarah (2: 22)

***Istithnaa*** *(*Maneno yenye kwenda nje ya hukmu hii):

Kusimama kwenye ة (taa marbuwtwah ya kike iliyofungwa) kunapelekea kutokuwepo hukmu hii ya مَدُّ الْعِوَض (maddul-'iwadhw) kwani wakati huo huondoka tanwiyn na kusimamiwa kwa ه (haa) saakinah[2]

Mfano:

مَّغْفِرَةً فَرِيضَةً زَكَوٰةً

[2] Rejea mlango wa 'Kusimama kwenye mwisho wa neno'